

Balozi wa Biko Tanzania, Kajala Masanja (kushoto), akikabidhi fedha Sh. milioni 10 kwa Nuru Mikikadi (katikati), aliyeibuka mshindi wa droo kubwa ya Bahati Nasibu ya Biko, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Uhusiano wa Benki ya CRDB Tawi la Premier Palm Beach, Flamiana Msilu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

NIPASHE UK 4.

# Chanzo cha vifo samaki Mto Mara chatajwa

## Na Mwandishi Wetu

**KAMATI** maalum iliyoundwa kuchunguza mabadiliko ya maji katika Mto Mara na kusababisha samaki kufa, imekamilisha kazi hiyo huku ikibainisha kuwa chanzo ni kinyesi cha mifugo, shughuli za binadamu na nguvu za asili.

Maji ya mto huo yalibadilika rangi na kuwa meusi kisha kutoa harufu na kusababisha idadi kubwa ya samaki kufa, hivyo kumlazimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano

na Mazingira, Dk. Selemani Jafu, kuunda kamati kuchunguza chanzo cha vifo hivyo.

Wajumbe wa kamati hiyo ni Dk. Kessy F. Kilulya, Mkuu wa Idara ya Kemia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Charles Kasanzu kutoka Idara ya Jiolojia UDSM, Daniel Ndio, Mkurugenzi wa Udhhibiti na Usimamizi wa Kemikali katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Renatus Shinhu, Mkurugenzi wa Bonde, Mamlaka ya Bonde la Maji Ziwa Victoria.

Wengine ni Mkurugenzi wa

Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRD) Kituo cha Mwanza, Baraka Sekadende, Dk. Neduvoto Molele kutoka Mamlaka ya Afya ya Mimea na Usimamizi wa Viatilifu (TPHPA), Ofisa kutoka Ofisi ya Rais Ikulu.

Yusuf Kuwaya kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara na Faraja Ngelageza, Mkurugenzi Msaidizi Bioanuai, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

Akitoa matokeo ya uchunguzi mjini Musoma, Mwenyekiti wa Kamati, Profesa Samuel Manyele, alisema hali hiyo imetokana na kuwapo kwa kiwango

kikubwa cha kinyesi cha mifugo pamoja na uozo wa mimea ndani ya mto hasa mimea vamizi kama vile magugu maji na matete. Prof. Manyele alisema hali hiyo ilisababisha kupungua kwa kiasi kikubwa kiwango cha oksijeni ndani ya mto, hivyo maji kubadilika rangi na kuwa na harufu mbaya, huku samaki wakikosa chakula na hatimaye kufa.

Hata hivyo, alikanusha picha zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilizokuwa zikionyesha samaki wakiwa wamekufa kwa wingi, akisema si kutoka Mto Mara.